**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

Mkuu wa shule : 0755961180/0674495493
M/Mkuu wa shule : 0769256548
Matroni : 0768111403
Shule ya Sekondari ; BUKARA.
S. L. P 1393,
Bukoba.
Tarehe ...................

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi
.....................................................
S. L. P ..........................................
.....................................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI BUKARA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOBA MKOA WA KAGERA MWAKA .......**

## 01. UTANGULIZI.

Nafurahi kukutaarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano, na atasoma tahasusi ya ........ katika shule hii mwaka .......... Shule ya sekondari Bukara ipo umbali wa kilometa 12 kutoka Bukoba mjini. Kutoka Bukoba mjini mwanafunzi itabidi apande gari zinazoelekea Maruku au Ntoma na kushuka kituo cha Kanyarwe. Nauli ni Tsh 2000/= kutoka Kanyarwe hadi shuleni kwa daladala,na, mwanafunzi itabidi apande bodaboda kwa Tsh 1000/=. Si busara kufika shuleni usiku.

Anatakiwa kuripoti shuleni tayari kwa kuanza muhula wa kwanza tangu tarehe _________ mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe __________ Akichelewa kuripoti shuleni zaidi ya wiki mbili bila sababu maalumu baada ya shule kufunguliwa, anaweza kupoteza nafasi yake. Siku za kuripori wanafunzi ni **Jumatatu mpaka Ijumaa kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 12:30 jioni.**

## 02. MAMBO YA KUZINGATIA

### 02.01. SARE YA SHULE.

**A.Wavulana**

Shati mbili nyeupe zenye mikono mirefu na mfuko mmoja kushoto, ndefu ya kuchomekea isiwe mtumba.

Suruali mbili za dark blue , urefu unao funika visigino, upana wa inchi 16, na zenye mifuko miwili pembeni kulia na kushoto na mfuko mmoja nyuma kulia ( usinunue modo/inayobana) na iwe na upindo chini (turn up).

Viatu vyeusi vya ngozi visiwe na visigino virefu, na viwe vya kamba.

Soksi nyeusi jozi mbili.

Sweta yenye rangi ya kijani iliyokolea na michirizi ya dark blue shingoni , mikononi na upindo wa chini ya sweta yenye muhuri wa shule inaweza kupatikana katika Duka la Shule Kwa shilingi 18000

**Tai ya dark blue yenye michirizi mieupe yenye nembo ya shule**

### B.Wasichana

Shati mbili nyeupe zenye mikono mirefu na mfuko mmoja kushoto, ndefu na ya kuchomekea

Sketi mbili dark blue zenye marinda box na urefu wa kufunika magoti ( zenye michirizi nyeupe/ufito mweupe WA kuzungushia)

Viatu vya ngozi vyeusi vya kama na visiwe na visigino virefu na visiwe bajaji ( bajaji haziruhusiwi)

Soksi nyeupe jozi mbili ndefu za kufunika miguu ( stockings) zisiwe fupi.

**NB**: Kwa upande wa **hijabu** iwe nyeupe na iwe ya kufunika mikono na sketi ifike miguuni yaani ndefu.

**Tai ya dark blue yenye michirizi mieupe**

Sweta yenye rangi ya kijani iliyokolea na michirizi shingoni ya blue, mikononi na upindo wa chini ya sweta yenye muhuri wa shule Unaweza kuipata shuleni kwa Tsh 18000

Mahitaji mengine ya Sare ni pamoja na:

(i) Shamba dress (Gauni) mbili kitambaa cha mikono mifupi za rangi ya pinki Kwa wasichana ,tisheti mbili kijivu hafifu iliyokoleza yenye nembo ya shule (Unaweza kuzipata katika Duka la Shule Kwa TSH 15000 Kila moja)Kwa na suruali jeusi kwa ajili ya kushindia Kwa wavulana. Kumbuka ,Urefu ni kuvuka goti kwa wakristo, na kwa waislamu ni kufunika miguu kwa urefu wa sentimeta 5. Na mshono wa gauni ni solo Kwa Wasichana .

(ii) Sare ya michezo kwa shule hii ni track suti jozi moja (1) rangi kijani iliyopauka yenye miraba myeupe (adidas) iliyochanganganya na rangi ya fedha(Silver) kwa ajili ya michezo na kwa baridi wakati wa kujisomea usiku yenye nembo ya shule. Sketi rangi ya nyeusi (kitambaa cha sukari) pia bukta pana kuvuka magoti rangi ya blue Kwa wasichana na wavulana, raba jozi moja (1), T-shirt ya kijani iliyopauka iliyochanganywa na rangi ya fedha nzito, yenye nembo ya shule, viatu vya michezo Kwa wavulana

(iii) Jacket moja (1) nzito nyeusi isiyo na kofia Kwa ajiri ya baridi wakati WA kujisomea usiku.(Isiwe na maandishi yoyote)

(iv) Tai blue jozi mbili (2) yenye michirizi midogo myeupe yenye nembo ya shule(Ili kuwa na Sare moja vifaa hivi vinapatikana katika Duka la shule kwa bei nafuu)

***NB:*** Ni muhimu mwanafunzi kuja na mwavuli kwani maeneo haya ni ya mvua nyingi. Mwanafunzi pia aje na tochi au taa ndogo za solar kwa ajili ya kumsaidia usiku pindi tu umeme unapokatika.

**02.02. MICHANGO YA SHULE.**

a) Ili kuhakikisha kwamba shule inaendelea kutoa huduma iliyo bora tunakuomba mzazi/mlezi kuchangia Michango ya uendeshaji wa shule.

**NB:** Michango yote ilipwe benki ya NMB akaunti namba ya shule 31801100077 Bukara **secondary .** Hakikisha unaandika jina la mwanafunzi kwenye pay-in-slip.

b) Michango inayotakiwa kulipwa kwa kila mzazi/mlezi ni kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:-

| Na | MICHANGO | KIASI (TSHS) | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 80,000/= | Lipia benki |

***MUHIMU: /*** Kila mwanafuzi aripoti shuleni akiwa na bima ya afya.

***Zingatia:***

- Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule namba **31801100077 BUKARA SECONDARY** (Benki ya NMB).
- Hakikisha unaandika jina la mwanafunzi kwenye pay-in-slip.
- Siku ya kuripoti hakikisha unaleta nakala za malipo (Bank pay-in-slip) na zikabidhiwe kwa muhasibu wa shule pindi tu ufikapo shuleni.
- Pamoja na fomu hii tunaambatanisha mchoro wa sare ya darasani ambayo ni kitambaa cha blue na gauni ya kushindia rangi ya damu ya Mzee Kwa wasichana (kitaambaa cha tetroni).
- Mzazi/mlezi unapotaka kuwasiliana na mwanafunzi awapo shuleni tumia namba za mkuu wa Shule au Matron.

**c) MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI NI:-**

a) Ream (A4) ya karatasi 2 kwa mwaka.
b) Madaftari makubwa counter book (quire 4) kumi (10).

c) Oxford Dictionary- Advance learners.
d) Kamusi ya Kiswahili.
e) Karamu za wino, za risasi, rula ,raba ,mkebe wa hisabati (Mathematics Set) na scientific calculator na Graph pad 1 yenye karatasi 50
f) Mashuka mawili (2) rangi ya pinki Kwa wasichana na blue Kwa wavulana, blanketi moja (1), mto pamoja na foronya moja (1) rangi ya pinki Kwa wasichana na blue Kwa wavulana, chandarua kimoja (1) rangi ya blue, godolo futi 2½ (super banco).
g) Vyombo vya chakula (sahani, bakuri, kijiko na kikombe).
h) Taulo Kwa wavulana na wasichana, kitenge kimoja cha kujifunga wakati wa kwenda kuoga Kwa wasichana tu.
i) Galeni/chombo chochote chenye uwezo wa kutunzia maji ya kunywa (lita 5 au zaidi).
j) Mafuta ya kujipaka, dawa ya meno, ndala, toilet paper (mikunjo 6) na dawa ya viatu.
k) Viatu vya wazi vyeusi vya kuvaa baada ya masomo.
l) Ndoo mbili za Lita 20 zenye mifuniko ,sabuni ya maji Lita 5 (Antiseptic Soap)Kwa ajiri ya usafi wa Choo
m) Mfagio wa chelewa wenye mpini mmoja, Hard bloom moja (brush ngumu yenye mpini), Soft bloom1 (brush nyepesi mfagio wa ndani), squeezer (mfagio wa kukaushia maji, reki 1, fyekeo 1 na kotama 1,jembe lenye mpini Kwa Wasichana wote ,Panga
   Kwa Wavulana Wa HGK na Shoka Kwa Wavulana Wa HGL
n) Picha (passport size) nne (4).

**d) MAHITAJI MENGINE YA KITAALUMA.**

Mwanafunzi anayeripoti ahakikishe analeta viambatanisho vya kitaaluma vifuatavyo kwa ajili ya matumizi ya ofisi:

(i) Nakala ya cheti halisi cha kuzaliwa (Birth certificate).
(ii) Nakala ya cheti cha kuhitimu kidato cha nne (Leaving certificate).
(iii)Nakala ya hati ya matokeo ya kidato cha nne (Results slip).
(IV)Faili moja Kwa ajiri ya kutunzia nakala za mitihani yake na mazoezi mbalimbali

***NB:*** Mzazi/Mlezi anashauriwa kumnunulia mwanafunzi japo kitabu kimoja kimoja kwa masomo atakayosoma hapa shuleni kulingana na tahasusi aliyopangiwa.

**e) MAHITAJI YA VITABU VINAVYOTAKIWA.**

Mzazi/mlezi kumbuka kwamba, ili mwanafunzi aweze kutimiza malengo yake ya kitaaluma, anapaswa pia awe anasoma vitabu. Unaombwa na **bodi ya shule** kumnunulia mwanao angalau **kitabu kimoja** kwa kila somo kulingana na masomo anayosoma (VITAKAGULIWA SIKU YA KURIPOTI SHULENI).

| S/N | SOMO | AINA YA KITABU |
|---|---|---|
| 01 | BIOLOGY | 1. New Understanding Biology For Advanced Level By Suzane Toole, Complete Advance Biology By Respicius R.<br>2. Biological by Taylor DJ, Adv. Manual |
| 02 | CHEMISTRY | 1. A-Level chemistry By EN. RAMSDEN<br>2. A-Level Physical Chemistry 6th Edition by HEYS.<br>3. Advanced1chemistry review by William W. Davies By MZUMBE BOOK PROJECT |
| 03 | GEOGRAPHY | 1. An interdrated approach by Waugh D.2009. Geography landscape appreciation By Mark night.<br>2. Practical Geography for Africa By S.M.Pritchand<br>3. Practical Geography A-Level by KAMILI Z.2011 |
| 04 | HISTORY | 1. Essential in Advanced level History –paper 1 by SALEHE YASIN<br>2. Essential in Advanced level History-paper 2 by SALEHE YASIN |
| 05 | KISWAHILI | 1. Fonolojia ya Kiswahili sanifu(FOKISA) sekondari na vyuo By MASSAMBA DPB na WENZAKE<br>2. Fasihi ya Kiswahili, chuo kikuu Huria cha Tanzania By MULOKOZI, MM 1996 |
| 06 | ENGLISH LANGUAGE | 1. The Real English Text Book For Advanced Level Form 5 & 6 By KADEGHE MICHAEL, 2010<br>2. Advanced English language, Form 5 & 6 By DSM OXFORD UNIVERSITY PRESS, 2012 |
| 07 | GENERAL STUDIES | 1. Understanding Advanced level General studies By JAMES BIGIRAMUNGU & SM. DEOGRATIAS 2012 |

## 03. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebiswa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na:

**03.01: Sheria na kanuni za shule.**

Sheria za shule zimewekwa ili kuwezesha kufikiwa kwa malengo ya taifa, shule na mwanafunzi mwenyewe. Hivyo mzazi/mlezi na mwanafunzi ambaye ndiye mlengwa haswa, anapaswa kuzisoma kwa makini, kuzitafsiri, kuzielewa na kuzitii wakati wote ili malengo yetu yaweze kufanikiwa kwa faida yetu sote. Sheria hizi ni kama zifuatavyo:-

(i) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

(iii) Kushiriki kwa makini kufanya maadalio ya jioni (preparation).

(iv) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(v) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako hapa shuleni.

(vi) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

(vii) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(viii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(ix) Kutunza mali za shule na za wengine na kujaza mkataba wa Ufaulu.

**MUHIMU.**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi au kuwasiliana na mzazi bila kibali maalumu toka ofisi ya Mkuu wa Shule na Mzazi hauruhusiwi kuwasiliana na mwanafunzi Kwa namba tofauti na zilizopo katika fomu hii.**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa mkuu wa shule (msiba/ugonjwa).**

**03.01. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI:-**

i. Wizi.
ii. Kutohudhuria masomo kwa siku 90 bila taarifa.
iii. Kugoma au kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
viii. Uvutaji wa sigara.
ix. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xi. Kushiriki matendo ya uharifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xiii. Kumiliki simu au kua na kifaa chochote cha simu, kukutwa au kutumia simu ya mkononi kwa mazingira ya shule.
xiv. Kudharau bendera ya taifa.
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua ama kunywa sumu n.k.
xvi. Uharibifu wa mali za umma kwa makusudi kuchafua rangi za madarasa na mabweni, kuaribu MIUNDOMBINU ya Shule ,kuvunja vioo kuvuna na Kula matunda ya Shule bila ruhusa.
xvii. Kukataa adhabu kwa makusudi.

**04. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKABIDHIWA SHULENI NA MWANAFUNZI PINDI TU ANAPORIPOTI.**

(i) Fomu ya kupimwa afya yake (Form For Medical Examination) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali.
(ii) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
(iii) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

***Nakutakia kila la kheri katika kufikia malengo yako!***

***"KARIBU SANA KATIKA JUMUIYA YA WASHINDI***

DAVID M.WILBARD
MKUU WA SHULE

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utaperi (wizi kwa njia ya mtandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHARI UPATAPO UJUMBE WOWOTE

KUHUSU MWANAFUNZI AU MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:-

- Mkuu wa shule : 0755961180
- Makamu Mkuu wa shule : 0768111403
- Mwandamizi Taaluma: 0753191029
- Mwanzamizi malezi: 0754384591
- Matroni: 0769256548

**FOMU NO. 1**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

## FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by a medical Officer in respect of all Form I and Form V entrants.
Student's full name ……………………………………………………………………………………
Age/Years …………………………………… Sex ……………………………………………………
Blood found (red and white) ………………………………………………………………………
Stool examination …………………………………………………………………………………
Urinalysis ……………………………………………………………………………………………
Venereal Diseases test ……………………………………………………………………………
Eye test ………………………………………………………………………………………………
Ears ……………………………………………………………………………………………………
Chest …………………………………………………………………………………………………
Spleen …………………………………………………………………………………………………
Abdomen ……………………………………………………………………………………………
Urine for Pregnant …………………………………………………………………………………

**ADDITIONALL INFORMATION** (If any) e.g. Physical defects, impairment(s) e.g. arm, leg etc. infection chronic or family disease etc.

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.

Signature …………………………
Designation ………………………
Stamp ………………………………

**FOMU NO. 2.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOBA**
**SHULE YA SEKONDARI BUKARA**

**FOMU YA KUKUBALI KUSOMA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA BUKARA**

**SEHEMU A: MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI** (Personal Particular)
(Jaza taarifa kwa umakini, usahihi na ukweli. Hii ni siri yako na mkuu wa shule tu)

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. JINA LA MWANAFUNZI (kama yalivyo kwenye vyeti vyako) …………………………………………………………
2. TAREHE YA KUZALIWA ………………………/…………………/……………………
3. MAHALI ULIPOZALIWA: MKOA…………………………WILAYA……………………… TARAFA…………………………KATA……………………KIJIJI/MTAA……………………
4. DINI……………………………DHEHEBU……………………KABILA………………………
5. SHULE NITOKAYO……………………………………………………NAMBA YA MTIHANI WA TAIFA KIDATO CHA NNE……………………………UFAHULU KIDATO CHA NNE: DIVISHENI……………………POINTI…………………………………
6. Jina kamili la Baba:…………………………………………Kazi ya baba…………………… Anwani……………………………Namba ya simu ……………………/……………………
7. Jina kamili la Mama……………………………………… Kazi ya mama………………… Anwani ……………………………Namba ya simu ……………………/……………………

**SEHEMU B: HABARI ZINAZOWAHUSU WAZAZI/WALEZI** (Ijazwe na Mzazi/Mlezi mwenyewe)

1. Jina la baba Mzazi/Mlezi……………………………………………………
   Anwani ………………………
   Namba ya simu (kiganjani)…………………………… Kazi ya baba Mzazi/Mlezi…………………………
   Mahali anakoishi kwa sasa: Kijiji/Mtaa………………………………………Wilaya………………………
   Mkoa …………
   Weka Passport size ………………………………………………………………………………………………
2. Jina la Mama Mzazi/Mlezi……………………………………………………Anwani……………………… Namba ya simu (kiganjani)…………………………… Kazi ya baba Mzazi/Mlezi……………………… Mahali anakoishi kwa sasa: Kijiji/Mtaa………………………………………Wilaya……………………… Mkoa ……………………………………………………………………………………………………………
3. Ndugu/Jamaa/ Marafiki wa karibu na muhimu wanaoweza kuwa msaada kwa mwanafunzi.
   Wafuatao ni ndugu/jamaa/rafiki zangu wa karibu ambao wanaweza kunisaidia kama kuna dharura . (ni vema wakawa watu wazima) weka Passport size zao

| Na. | Jina la ndugu/jamaa/rafiki | Anwani ya anapopatikana | Simu (inayopatikana) | Uhusiano |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |

***Angalizo:*** Ni ndugu hao (walioandikwa hapa juu na wazazi/walezi) tu watakaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi hapa shuleni kwa tarehe na muda utakaopangwa na uongozi wa shule kisha wazazi/walezi kutaarifiwa. (Ambatanisha picha passport size zao)


4. Ripoti za maendeleo yake kutoka shuleni ziwe zinatumwa kwa:
   Ndugu…………………………………………… Anwani ya posta S. L. P …………………………………
   Simu ……………………………Mahusiano yake na mwanafunzi ……………………………………………
5. Mwanafunzi ni mfuasi wa Dini/Dhehebu la ………………………………………………………………
6. Kituo cha Basi/Trani kilichopo na nyumbani ni …………………………………………………………
7. Namba yangu ya simu kwa mawasiliano ya haraka ni ……………………………………………………
8. Mimi ……………………………………………………… Bila kushinikizwa na mtu yeyote, nikiwa na akili timamu ninakubali kusoma katika shule ya sekondari Bukara katika Tahasusi ya ……………………na ninahaidi kusoma na kujifunza kwa bidii ili niweze kufikia malengo yangu, ya shule na ya Taifa.
   Pia ninahaidi kutojihusisha kwa aina yoyote kwenye mgomo, fujo au kosa lolote la jinai.
   Saini ya mwanafunzi ……………………………………………tarehe ………………………………………
9. Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi)…………………………………………………… nimeridhia mwanangu asome Tahasusi aliyopangiwa ambayo ni ……………………………… katika shule ya sekondari Bukara. Vile vile ninahaidi kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi bora ya mwanangu. Na ninakubaliana na sheria za shule na kanuni zake, nitalipa ada na michango ya shule kama ilivyoainishwa na kwa muda mwafaka (mapema) ili kuwezesha shughuli za shule ziweze kufanyika kama zilivyopangwa.


   Saini ya Mzazi/Mlezi………………………Tarehe ………………………

DAVID M WILBARD
MKUU WA SHULE

Tarehe ………………………

## MSHONO WA SARE YA SHULE







Sketi ya darasani dark blue Sketi ya michezo nyeusi Kitambaa cha sukari

Gauni la kushindia (shamba dress)
Rangi ya damu ya mzee
Kitambaa cha tetroni+

1-Mbele



2-Nyuma




N.B: Hakikisha urefu wa gauni unavuka kwenye magoti. (isiwe chini ya sentimita 15.)